TAASISI YENYE VIWANGO VYA UBORA VYA ISO 9001:2015

# THE Regulator

LINATOLEWA BURE. HALIUZWI

TANZANIA SENSA 23 Agosti 2022 Jiandae Kuhesabiwa

ISSN: 0856 -8030 | TOLEO NA 2/2022 Aprili - Juni 2022

Jarida la kila robo mwaka la Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania



## Vipaumbele sekta ya Mawasiliano 2022/2023

- Tanzania yasifiwa utayari usimamizi wa kushirikiana
- Wasichana wahamasishwa kusoma TEHAMA
- Kushuka gharama kwabadili mwelekeo matumizi simu za mkononi

# OFISI ZA MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA




## MAKAO MAKUU

Mawasiliano Towers
20 Barabara ya Sam Nujoma
S.L.P 474
**14414 DAR ES SALAAM**
Simu : +255 22 2199760 - 9
+255 22 2412011 - 2
+255 784558270 - 1
Nukushi : +255 22 2412009 -10
Baruapepe : dg@tcra.go.tz
Tovuti : www.tcra.go.tz

## Ofisi ya Zanzibar na Ofisi za Kanda

### Ofisi ya Zanzibar
Na. 19 Mbuyukisutu,
S.L.P 3284,
**71194 Mjini Magharibi, Zanzibar**
Simu: 255 24 2235062,
Baruapepe: zanzibar@tcra.go.tz

### Kanda ya Kaskazini
PSSPF Plaza, Ghorofa ya sita
Barabara ya Old Moshi
S.L.P 15675,
**23194 Arusha.**
Simu: +255 272970286
Baruapepe: arusha@tcra.go.tz

### Kanda ya Kati
LAPF Plaza, Ghorofa ya nne
Na. 2 Mtaa wa LAPF
S.L.P. 2229,
**41194 Dodoma.**
Simu: +255 262321731
Baruapepe: dodoma@tcra.go.tz

### Kanda ya Nyanda za Juu Kusini
Jengo la NHIF, Ghorofa ya tano
Na. 7 Barabara ya Karume,
S.L.P 1375,
**53194 Mbeya,**
Simu: +255 25 250 5016
Baruapepe: mbeya@tcra.go.tz

### Kanda ya Ziwa
Jengo la NSSF Mafao, Ghorofa ya nne,
upande wa B,
Na. 13 Barabara ya Jomo Kenyatta
S.L.P 3108,
**32194 Mwanza.**
Simu: +255 (0)28 2505082,
Baruapepe: mwanza@tcra.go.tz

### Kanda ya Mashariki
Na. 147 Barabara ya Kajenge,
S.L.P 35615,
**14194 Dar es Salaam.**
Simu +255 22 2775110
Baruapepe: easternzone@tcra.go.tz

KISWAHILI

Namba ya Usajili: 00000115
Aprili - Juni 2022
ISSN: 0856-8030

Hii ni sehemu ya Kiswahili ya jarida la The Regulator, linalotolewa mara nne kwa mwaka na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), taasisi ya serikali inayosimamia mawasiliano ya kielektroniki na posta nchini. Jarida hili ni sehemu ya utekelezaji wa majukumu ya Mamlaka.

### Anwani ya ofisi za uhariri:

Jengo la Mawasiliano,
Na. 20 Barabara ya Sam Nujoma,
S.L.P 474, Postikodi 14414 Dar es Salaam.
Simu: +255 784558270, +255 784558271.
Barua pepe: regulator.magazine@tcra.go.tz.

## Bodi ya Uhariri

**Mwenyekiti/ Mhariri**
Dkt. Emmanuel Manasseh
**Mhariri/ Mratibu**
Ms. Lucy Mbogoro
**Wajumbe**
Dr. Philip Filikunjombe
Bw. Semu Mwakyanjala
Bi. Thuwayba Hussein
Bw. Abel John
Bw. Brian Kalinga
Bi. Sophia Nahoza
Bw. Noah Laltaika
Bw. Peter Kihogo
**Mhariri wa Uzalishaji**
Bw. Isaac Mruma

## Yaliyomo

2 | Kutoka Mkurugenzi Mkuu
3 | Mashauriano TCRA na wadau kuendeleza sekta
4 | Raslimali za mawasiliano kwa wavumbuzi
5 | Takwimu: Kushuka gharama na mwelekeo upigaji simu
6 | Wasichana wahimizwa kusoma sayansi, teknolojia
8 | Vipaumbele vya Serikali sekta ya Mawasiliano 2022/2023
14 | Vikoa vya dot tz (.tz)



**PICHA YA JALADA**
*Rais Samia Suluhu Hassan akipata maelezo kuhusu Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania kutoka kwa Mkuu wa kitengo cha Mawasiliano TCRA, Bi. Lucy Mbogoro kwenye banda ya TCRA katika maonyesho yaliyokuwa sehemu ya maadhimisho ya Siku ya Uhuru wa Vyombo vya Habari Duniani kitaifa Arusha 3 Mei 2022. Katikati ni Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mhe. Nape M. Nnauye (Mb). TCRA inasimamia sekta ya utangazaji Tanzania Bara.*

THE Regulator

## Barua ya Mhariri

### Tanzania juu kwa juu kidijitali

Makala kuu kwenye toleo hili inaainisha vipaumbele vya Serikali katika sekta ya mawasiliano kwa mwaka wa fedha 2022/2023. Maeneo ya kimkakati yaliyopewa kipaumbele ni pamoja na kuendeleza mkongo wa taifa wa mawasiliano, nguvu zaidi katika kutekeleza mpango wa Tanzania ya kidijitali na kuweka miundombinu katika maeneo mengi zaidi ya vijijini na yale yasiyofikika kwa urahisi.

Tumechapisha takwimu za kipindi cha mwaka mmoja kati ya April 2021 na Aprili 2022 ambazo zinaonyesha kukua kwa kasi kwa huduma na mwelekeo wa matumizi. Eneo pekee lililoonyesha kushuka ni utumaji na upokeaji wa barua na vifurushi kupitia Shirika la Posta Tanzania; sababu zikiwa ni pamoja na maendeleo ya kasi ya teknolojia ya Habari na Mawasiliano na kuzuka kwa janga la UVIKO-19 ambalo liliathiri usafirishaji kimataifa.

Tunayo Makala ya usimamizi wa ushirikiano ambapo Tanzania, kupitia TCRA, imetajwa kama kinara wa utekelezaji wa mfumo huo barani Afrika.

Maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Wasichana na TEHAMA, Aprili 28 yalikuwa na mvuto wa kipekee kutokana na uvumbuzi kwenye maeneo mengi uliofanywa na wanafunzi wasichana.

*Mhariri anakaribisha makala na picha kuhusu masuala mbalimbali ya sekta ya mawasiliano. Makala zisizidi kurasa nne (4) za ukubwa wa A4, zikiwa kwenye maandishi ya Times New Roman, fonti 12 na ziwe na uasili. Picha ziwasilishwe kwa mfumo wa JPEG.*

Ujumbe wa Mkurugenzi Mkuu

# Teknolojia za Kidijitali na Afya Bora kwa Watu wa Umri Mkubwa

**Ujumbe huu ulitolewa na Mkurugenzi Mkuu wa TCRA tarehe 17 Mei, 2022; Siku ya TEHAMA Ulimwenguni. Umefupishwa na kurekebishwa kwa ajili ya jarida hili.**

Tarehe 17 Mei kila mwaka inaadhimishwa kama kumbukumbu ya siku ya kusainiwa mkataba ulioasisi Shirika la Umoja wa Mataifa linalosimamia mawasiliano (ITU). Lilianzishwa kuwezesha mataifa kuunganishwa katika mitandao ya mawasiliano na kusimamia mgawanyo wa masafa ya redio kimataifa na obiti za setilaiti.

Majukumu mengine ni kuendeleza viwango vya kiufundi vinavyohakikisha mitandao na teknolojia inaunganishwa bila vikwazo, na kuboresha kupatikana na kuchukuliwa kwa matumizi kwa TEHAMA kwa jamii ambazo hazihudumiwi ipasavyo katika maeneo yote ulimwenguni.

Kaulimbiu ya mwaka huu – "Teknolojia za Kidijitali na Afya Bora kwa Watu wa Umri Mkubwa", inasisitiza umuhimu wa matumizi ya TEHAMA katika kufikia uzee wenye afya kwa kuwezesha teknolojia zinazopatikana kwa urahisi zinazohakikisha ushirikishwaji wa wazee bila kujali eneo au mahali walipo.

Matumizi ya TEHAMA yameiwezesha nchi kufikia ukuaji wa uchumi. Aidha ina nafasi kubwa ya kubadilisha maisha ya wazee, hasa katika kuboresha maendeleo vijijini kwa kuongeza wigo wa upatikanaji wa taarifa.

Kaulimbiu hii ni wito kwa wahusika katika sekta ya mawasiliano kuzingatia na kuhakikisha kwamba maendeleo ya teknolojia yanazingatia mahitaji ya wazee na kukuza uzee wa afya katika jamii kwa ujumla.

TCRA imedhamiria kuweka mazingira ambayo wadau wa sekta ya mawasiliano Tanzania wanaweza kuendelea kutoa huduma bora kwa makundi yote ya jamii wakiwemo wazee.

Vilevile, TCRA itaendelea kusimamia sekta ya mawasiliano ili kuhakikisha inatoa huduma muhimu katika maeneo yote ya nchi ikiwa ni pamoja na vijijini na kuwafikia wazee ambao wengi wao wanaishi vijijini.




*Mkurugenzi Mkuu wa TCRA, Dr. Jabiri K. Bakari ( katikati) katika kikao cha wadau Kanda ya Ziwa jijini Mwanza hivi karibuni. Kulia ni Mkuu wa Kanda hiyo, Mhandisi Francis Mihayo na kushoto ni Mkuu wa Masuala ya Wateja na Watumiaji, Makao Makuu, Bw. Thadayo Ringo.*

Mfumo wa utoaji leseni wa Tanzania unaosimamiwa na TCRA unahakikisha na kuruhusu huduma na teknolojia mtambuka; suala linaloongeza wigo kwa watoa huduma kuongeza ubunifu na kuwezesha kupenya kwa huduma za kiteknolojia maeneo yote ya nchi.

Mfumo wa leseni unaoingiliana kihuduma na kiteknolojia unarahisisha watoa huduma za mawasiliano kufikisha huduma mtambuka zenye manufaa kwa wazee kote Tanzania.

Watu waliounganishwa vema na TEHAMA wanaweza kufanya kazi na kuwasiliana kutoka popote kwenye sayari-dunia. Wanaweza kupata na kutoa taarifa na kupata zana za kujifunzia, na kuboresha biashara zao.

Faida hizi na nyingine tumezishuhudia wakati wa janga la UVIKO-19 kuanzia mwaka 2019.

TCRA itaendelea kushirikiana na wadau kwa kuzingatia fursa mbele yao na changamoto zinazowakabili wazee wanapotumia teknolojia za kidijitali ili kuhakikisha kuwa wananchi wananufaika na TEHAMA.

Tunawahimiza watoa huduma za mawasiliano kuendelea kuwekeza katika miundombinu ya TEHAMA na utoaji wa huduma zinazohusiana na TEHAMA zenye kuwagusa wazee.

TCRA, msimamizi wa mawasiliano Tanzania, inafurahi kuona kwamba baadhi ya watoa huduma wanatekeleza hili.

# Mashauriano TCRA na wadau kuboresha huduma, kuendeleza sekta

**Na Mwandishi Wetu**

Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania imeanzisha utaratibu wa kukutana na wadau wa sekta ya mawasiliano kwenye kanda mara kwa mara ili kujadiliana namna ya kuboresha sekta hiyo.

Kikao-kazi cha hivi karibuni kimefanyika Mwanza mwishoni kwa Mei 2022 kwa kushirikisha wadau wa Kanda ya Ziwa ambako TCRA imesisitiza kwamba itahakikisha watoa huduma za mawasiliano wanazingatia ubora na ufanisi na itashirikiana na vyombo vingine kujenga imani ya watumiaji katika huduma wanazopata.

Mkurugenzi Mkuu wa TCRA Dkt Jabiri K. Bakari aliwaambia wadau hao kuwa Mamlaka itashirikiana na wadau wengine wa usalama mtandaoni kuhakikisha usalama wa watumiaji.

Lengo ni kujenga imani katika huduma zinazotolewa na kuwafanya watumiaji wajisikie huru kutumia huduma hizo bila kuwa na wasiwasi wa usalama wao wakati wote wanapokuwa mtandaoni, alisisitiza.

Kikao-kazi hicho kilihusisha watoa huduma za utangazaji wa redio, televisheni na mitandao, televisheni za waya na watoa huduma za mawasiliano ya simu.

Wengine ni wamiliki wa kampuni za usafirishaji wa vifurushi na vipeto, watoa huduma za intaneti pamoja na umoja wa mafundi simu Kanda ya Ziwa.

Akitoa ufafanuzi kuhusu usalama mtandaoni, Mkurugenzi Mkuu Jabiri alidokeza kwamba mbinu za wahalifu zimebadilika; wametoka kwenye kutenda uhalifu katika mazingira ya kawaida na kuhamia mtandaoni.

Alitoa mfano wa utapeli unaofanywa kwa njia ya simu za mkononi.

"Kwa hiyo jinsi inavyoendelea na sisi lazima tuendelee na kujiongeza. Tulitoa maelekezo kuwa watoa huduma za mawasiliano ya simu lazima wawasiliane na wateja wao kwa kutumia namba 100. Hivyo ukipata taarifa ya simu kwa namba nyingine na ukakubaliana na matakwa ya aliyekupigia maana yake kuna tatizo," alisisitiza Mkurugenzi Mkuu.

Aliongeza kuwa TCRA inashirikiana na Jeshi la Polisi kuhakikisha mazingira ya mawasiliano kwenye mtandao yanaendelea kubaki salama kwa kila mtumiaji wa huduma.

"Wahalifu wanavyobadilika na sisi tunabadilika. Uhalifu mtandaoni ni uhalifu kama mwingine; kwa hiyo taarifa za uhalifu kwenye mtandao zinapaswa kwenda kwenye Kituo cha Polisi ambao wana Kitengo mahsusi cha kushughulikia uhalifu mtandaoni.

Baadhi ya washiriki wa kikao hicho walitaka ufafanuzi wa namna TCRA inavyodhibiti uhalifu mtandaoni.

Kuhusu faragha ya taarifa za mtumiaji wa huduma za mtandao, Mkurugenzi Mkuu alibainisha kuwa usalama wa taarifa za mtumiaji wa huduma za mtandao unalindwa kwa mujibu wa Sheria ya Makosa Mtandaoni.

Aliongeza kwamba mchakato wa sheria kamili itakayolinda faragha za mtumiaji wa huduma za mawasiliano unaendelea na matarajio ni kuwa itaanza kutumika hivi karibuni.

Aidha, aliwaeleza wadau hao kuwa TCRA inaandaa dirisha maalum kwenye tovuti yake ambalo litakuwa kama kituo cha taarifa cha kimtandao, na kitaitwa Tanzanite portal. Kitatoa taarifa mbalimbali zinazohusu sekta ya mawasiliano kwa watoa huduma, watumiaji na wadau wengine wa sekta ya mawasiliano.

Ameongeza kwamba TCRA imeboresha dawati la huduma kwa mteja lililopo makao makuu Dar es Salaam. Huduma hiyo itafikishwa kwenye ofisi za kanda. Mamlaka ina ofisi Zanzibar na kwenye zanda za Mashariki (Mikocheni Dar es Salaam), Kaskazini (Arusha) Kati (Dodoma), Nyanda za Juu Kusini (Mbeya), Ziwa (Mwanza).

"Ninyi watoa huduma ndiyo wateja wetu, lakini na ninyi mnao wateja mnaowahudumia. Kwa hiyo tumeboresha huduma kwa kuweka mazingira wezeshi; tumeweka fursa ambayo sasa unaweza kupata fursa ya kujadiliana masuala ya sekta na wahandisi, wanasheria, na wachumi wakakushauri zaidi jinsi ya kuboresha na kupanua huduma unazotoa na kuongeza tija ili kuwahudumia wananchi katika sekta pana ya mawasiliano.

# Raslimali za Mawasiliano kwa Wavumbuzi

Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) inatoa bure raslimali za mawasiliano kwa wavumbuzi katika TEHAMA/ dijitali (wabunifu wanaoanza) ili kutathmini manufaa ya bidhaa mpya za TEHAMA zilizovumbuliwa, na utafiti kwenye teknolojia zinazoibuka.

### Raslimali za Mawasiliano zinazotolewa na TCRA

Raslimali za mawasiliano zinazotolewa na TCRA kwa ajili ya majaribio ni pamoja na Raslimali za Namba (Huduma za ziada na misimbo ya USSD, kikoa cha dot tz (.tz) na masafa ya mawasiliano.

Muda wa Kutumika kwa Raslimali hizi za Mawasiliano

Raslimali hizi za mawasiliano zinaweza kutumika kwa miezi mitatu kuanzia pale zinapotolewa kwa mhusika na kuna uwezekano wa kuongeza muda huo iwapo aliyepewa raslimali hizo anataka kuongezewa.

Utaratibu wa kupata raslimali za mawasiliano kutoka TCRA kwa majaribio ya huduma

Mvumbuzi anayeanza anatakiwa:

i. Kupata idhini ya Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH)

ii. Kuwasilisha TCRA maombi ya raslimali za mawasiliano anazohitaji, na kuambatanisha nyaraka zifuatazo:

i. Barua ya Maombi,

ii. Idhini ya COSTECH,

iii. Nakala iliyothibitishwa kisheria ya Kitambulisho cha Taifa cha mwombaji,

iv. Nakala iliyothibitishwa kisheria ya Cheti cha Usajili wa Kampuni,

v. Andiko la wazo au eneo la uvumbuzi linaloombewa.

### Masharti ya kutoa Raslimali za Mawasiliano

i. Mvumbuzi anayetaka kutumia raslimali za mawasiliano zilizotengwa na TCRA kwa ajili ya majaribio anatakiwa kuziomba rasmi.

ii. Mwombaji anaweza kuwa mtu binafsi, kampuni na/au taasisi.

iii. Mwombaji atawasilisha kwa Mamlaka (TCRA) barua ya kuomba raslimali za mawasiliano, akiainisha matumizi yanayotarajiwa, mahali na huduma, tarehe ya kuanza kwa majaribio, na kuambatanisha idhini ya COSTECH.

iv. TCRA itaendelea kuwa na haki ya kutoa raslimali zilizoombwa kutegemea upatikanaji wake na matumizi yake.

v. Kwa vyovyote vile, anayepewa raslimali hizo kwa muda hatakuwa na haki ya kumilki raslimali alizopewa. Kila shughuli inayoombewa inatakiwa kuwa kwa majaribio na kwa kipindi kitakachotajwa.

vi. Raslimali zilizotolewa kwa muda zitatumika tu kwa madhumuni zilizoombewa.

vii. Kutolewa kwa raslimali yoyote ile, isipokuwa tu pale ilivyoelekezwa vinginevyo wakati wa kutolewa, kutakuwa kwa miezi mitat (3) tu kuanzia tarehe zilipotolewa.

viii. Anayepewa raslimali hizo anatakiwa kusitisha matumizi yake baada ya hiyo miezi mitatu.

Kwa maelezo zaidi, wasiliana na:

Mkurugenzi Mkuu
Jengo la Mawasiliano,
Na. 20 Barabara ya Sam Nujoma,
S.L.P 474,
Postikodi 14414 Dar es Salaam.
Simu: +255 784558270,
+255 784558271.
Barua pepe: dg@tcra.go.tz

## TAKWIMU

# Muda wa simu kwenda mitandao mingine waongezeka asilimia 400 ndani ya miaka mitano

Gharama za chini za kuunganisha simu kati ya mitandao ya simu za mkononi Tanzania zimewafanya watumiaji wengi zaidi kupiga simu mitandao mingine ukilinganisha na mitandao yao, takwimu zilizotolewa hivi karibuni na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania zinaonyesha.

Dakika za watumiaji kwenda mitandao mingine zimeongezeka sambamba na kushuka kwa viwango vya kuunganisha simu kati ya mitandao kati ya 2018 na 2022.

Takwimu kati ya 2018 na 2022 zinaonyesha wastani wa dakika kwenda mitandao mingine zimeongezeka kwa asilimia 400; kutoka 17 mwaka 2018 hadi 85 na imepungua kwenye mitandao ya watumiaji kwa asilimia 19.8; kutoka 101 mwaka 2018 hadi 81 mwaka; na kuongezeka kwa dakika mojahadi 82 Machi 2022.

Kwa kipindi cha mwaka mmoja; kati ya 2020 na 2021; wastani wa dakika kwa mtumiaji wa mitandao mingine uliongezeka kwa asilimia 51.8, kutoka dakika 56 hadi 85. Kipindi hicho kilikuwa na ongezeko la asilimia 1.2, kutoka dakika 81 hadi 82.

Kiwango cha kuunganisha simu kati ya mitandao ni gharama ambazo mtandao mwingine unatozwa kupitishia na kufikisha simu za maongezi kwenye mtandao mwingine. Hivi sasa ni shilingi mbilli (2.0); kutoka shilingi 15.60 mwaka 2018. Viwango hivi vinaanza kutumika Januari ya kila mwaka; na vya sasa vilipangwa Desemba 2017 kama sehemu ya mapitio ya kila miaka mitano ambayo yanatarajiwa kufanyika mwaka huu.

Jedwali 1: Mwelekeo wa gharama za kuunganisha simu kati ya mitandao na wastani wa dakika za kwenye mitandao ya watumiaji na kwenye mitandao mingine – 2016 -2022

| Mwaka | 2018 | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 |
|---|---|---|---|---|---|
| Kiwango cha kuunganisha (shilingi) | 15.60 | 10.40 | 5.20 | 2.6 | 2.0 |
| Dakika kwa watumiaji kwenye mitandao yao | 101 | 100 | 95 | 81 | 82 |
| Dakika kwa watumiaji kwenye mitandao mingine | 17 | 20 | 37 | 56 | 85 |

Kuenea kwa huduma za simu za mkononi, ambako kunapimwa kwa asilimia ya watumiaji ya uwiano wa watumiaji na idadi ya watu nchini, kumeongezeka kwa asilimia 11 katika miaka mitano; na huduma za intaneti zinachukuliwa kwa matumizi na karibu nusu ya Watanzania wote.

Jedwali 2: Kuenea kwa simu za mezani na za mkononi – 2016 hadi Machi 2022


| Mwaka (Machi)) | 2016 | 2017 | 2018 | 2019 | 2020 | 2021 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Za mezani | 129,597 | 127,094 | 124,238 | 76,288 | 72,469 | 71,834 |
| Mkononi | 40,044,186 | 39,953,860 | 43,497,261 | 49,143,053 | 51,220,233 | 54,044,384 |
| Jumla | 40,173,783 | 40,080,954 | 43,621,499 | 49,219,341 | 51,292,702 | 54,116,218 |
| Kuenea | 80% | 78% | 81% | 88% | 89% | 91% |

Jedwali 3: Makisio ya watumiaji wa intaneti: 2016 – 2021

| Mwaka | 2016 | 2017 | 2018 | 2019 | 2020 | 2021 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Watumiaji | 19,862,525 | 22,995,109 | 23,142,960 | 25,794,560 | 28,470,506 | 29,858,759 |
| Kuenea | 40% | 45% | 43% | 46% | 49% | 50% |

Jedwali 4: Laini za simu, watoe huduma wenye leseni na mwelekeo wa watumiaji: Aprili 2021 – Aprili 2022

| Maelezo | Aprili 2021 | Aprili 2022 | Asilimia ya ongezeko |
|---|---|---|---|
| Laini za simu zilizosajiliwa | 52,965,816 | 55,365,239 | 4.5% |
| Akaunti za pesa simu za mkononi | 27,326,938 | 35,749,294 | 30.8% |
| Watoa huduma kutumia miundombinu | 19 | 23 | 21.1 |
| Watoa huduma za program tumizi, huduma za ziada | 66 | 102 | 54.2 |
| Televisheni mtandaoni | 552 | 663 | 20.1 |



# Wasichana wahimizwa masomo ya sayansi, teknolojia

***Siku ya kimataifa ya wasichana na TEHAMA inaadhimishwa kila Alhamisi ya nne ya mwezi Aprili kwa lengo la kuwahamasisha wanafunzi wasichana kupenda na kuchukua masomo ya sayansi, teknolojia,uhandisi na hisabati, au kwa kifupi STEM - science, technology, engineering, mathematics. Makala hii ya picha inaonyesha namna maadhimisho ya mwaka huu yalivyofanyika, chini ya usimamizi wa TCRA.***

## SIKU YA KIMATAIFA YA WASICHANA NA TEHAMA, 2022

### Kuchukuliwa kwa matumizi na Usalama



*Wanafunzi wa shule mbalimbali za wasichana mjini Dar es Salaam wakiwa kwenye ukumbi wa Chuo Kikuu cha Dar Es Salaam kwa maadhimisho.*




*Baadhi yao walituzwa kwa ubunifu katika sekta ya TEHAMA. Kutoka kushoto ni Mkurugenzi Mkuu wa TCRA, Dkt. Jabiri K. Bakari; Mkurugenzi wa Idara ya Sayansi na Ubunifu, Wizara ya Elimu Prof. Maulito Kipayula, Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya TEHAMA, Dkt. Nkunde Mwasaga. Kulia kabisa ni Afisa wa TCRA, Mhandisi Beatrice Lema.*



*Wanafunzi wa shule ya Sekondari ya Wasichana Kilakala, Morogoro wakipatiwa maelezo kuhusu kilimo cha mboga kidijitali walipotembelea Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine (SUA) kama sehemu ya maadhimisho ya Siku hiyo.*

## MIFANO YA KUIGWA

Baadhi ya wasichana wa zamani waliochangamkia fursa za kusoma sayansi, teknolojia,uhandisi na hisabati na kufanikiwa maishani walitoa hamasa kwa washiriki.




*Cecylia Gellejah, Rubani, Air Tanzania*




*Khadija Mkocha, Mratibu, taasisi ya SMARTGIRLS*

# Vipaumbele vya Serikali sekta ya Mawasiliano 2022/2023

***Sehemu ya hotuba ya Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari Mhe. Nape M. Nnauye (Mb.) akiwasilisha Bungeni tarehe 18 Mei 2022 makadirio ya mapato na matumizi ya fedha kwa mwaka wa fedha 2022/23.***

Sekta ya Mawasiliano imeendelea kukua, takwimu zinaonyesha kuwa laini za simu zilizosajiliwa zimeongezeka kutoka **52,965,816** Mwezi Aprili, 2021 hadi kufikia laini **55,365,239** Mwezi Aprili, 2022 sawa na ongezeko la asilimia 4.5. Watumiaji wa intaneti wameongezeka kutoka **Milioni 29.1** Mwezi Aprili, 2021 hadi kufikia **Milioni 29.9** Mwezi Aprili, 2022 sawa na ongezeko la asilimia 2.7.Watumiaji wa huduma za kutuma na kupokea pesa kwa njia ya mtandao wa simu wameongezeka kutoka 27,326,938 Mwezi Aprili, 2021 hadi kufikia 35,749,298 mwezi Aprili, 2022 sawa na ongezeko la asilimia 30.8. Aidha, Watoa huduma wa Miundombinu ya Mawasiliano wamefikia 23 ukilinganisha na watoa huduma 19 Mwezi Aprili, 2021 (hii ni sawa na ongezeko la asilimia 21.1).

Watoa huduma wa huduma za ziada (Application Services and Value Added Services) wamefikia **102** ukilinganisha na **watoa huduma 66** Mwezi Aprili, 2021 (ongezeko la asilimia 54.5). Pia, Bei ya mwingiliano kati ya watoa huduma (Voice interconnection Charges) imeshuka kutoka Shilingi 2.6 kwa dakika mwaka 2021 hadi Shilingi 2.0 kwa dakika mwaka 2022 (punguzo la asilimia 23.1). Vituo vya kurusha matangazo ya redio vimeongezeka kutoka vituo 200 mwaka 2021 hadi kufikia vituo 210 Mwezi Aprili, 2022 na vituo vya kurusha matangazo ya runinga vimeongezeka kutoka vituo 50 mwaka 2021 na kufikia vituo 56 Mwezi Aprili, 2022.

Cable Television zimeongezeka kutoka 40 Mwezi Aprili, 2021 na kufikia 59 Mwezi Aprili, 2022 na magazeti yameongezeka kutoka 272 na kufikia 284 Mwezi Aprili, 2022. Serikali imeendelea kuweka mazingira rafiki ya matumizi ya teknolojia za Utangazaji hasa maudhui mtandaoni ambayo pia yamechangia kuongeza ajira kwa vijana. Hadi kufikia Mwezi Aprili, 2022 televisheni mtandao zimeongezeka kutoka 552 hadi 663 sawa na ongezeko la asilimia 20.1, blogu zimeongezeka kutoka 134 hadi 148 sawa na ongezeko la asilimia 10.4 na redio mtandao zimeongezeka kutoka 25 hadi 27 sawa na ongezeko la asilimia 8.0.

Takwimu za mwezi Aprili, 2022, zinaonesha kuwa asilimia 95 ya Watanzania wapo kwenye maeneo yenye mtandao wenye uwezo wa kutoa huduma za simu za sauti na jumbe fupi, yaani 2G network kupitia minara 12,228. Aidha, asilimia 68 ya Watanzania wapo kwenye maeneo yenye Mtandao wenye uwezo wa kutoa huduma za intaneti ya kasi ya 3G kupitia minara 11,753 na asilimia 45 wapo kwenye maeneo yenye Mtandao wa 4G kupitia Minara 6,656.

Hata hivyo pamoja na kwamba asilimia 68 wapo kwenye maeneo yenye huduma ya intaneti, ni asilimia 27 tu ya watumiaji wa huduma za mawasiliano wenye simu janja au vifaa vingine vya mawasiliano (laptop, tablets, iPad, n.k.) vyenye uwezo wa kutumia intaneti. Jitihada za serikali kuondoa kodi kwenye vifaa vya simu katika mwaka wa fedha 2021/22, pamoja na watoa huduma kutengeneza taratibu mbalimbali za kuwakopesha wateja wao simu kumeongeza idadi ya simu janja kwa takribani asilimia 2 tu kulinganisha na mwaka uliopita.

Matumizi ya TEHAMA pamoja na teknolojia zinazoibukia kama Artificial Intelligence (AI), Internet of Things (IoT), Blockchain na nyinginezo yanawezesha ujenzi wa miji ya kisasa na endelevu. Haya yote yanahitaji miundombinu thabiti na intaneti ya kasi. Upatikanaji na utumiaji wa huduma ya intaneti ya 4G kwa wananchi wengi unatarajiwa kuleta mageuzi makubwa katika uchumi wa kidigiti. Serikali imeendelea kuweka mazingira wezeshi kwa watoa huduma/wawekezaji

kujenga Miundombinu ya Mawasiliano ya Intanenti ya kasi ili kuongeza wigo (coverage) wa mitandao na kuimarisha ubora wa huduma za Mawasiliano ili kufikisha intaneti ya kasi kwa asilimia 80 ya Watanzania ifikapo mwaka 2025.

Pamoja na uwezo wa kuridhisha wa Intaneti ya 4G na uwekezaji unaondelea, Serikali kupitia TCRA imeshachukua hatua za kutengeneza Mkakati wa kuchochea miundombinu inayowezesha intaneti ya kasi ya 5G. Mkakati huu unahusisha pamoja na mambo mengine kupanga na kuweka masafa yatakayowezesha uwekezaji kwenye mitandao ya 5G. Serikali kupitia TCRA ipo tayari kutoa

Masafa kwa watoa huduma ambao wangependa kufanya majaribio ya teknolojia ya 5G (5G Trials). Utaratibu wa kugawa masafa yaliyobainishwa kutumika kwa teknolojia ya 5G utakuwa wa ushindani (Transparent & Competitive Process).

Katika Mwaka wa Fedha 2021/22 Wizara katika Eneo la Mawasiliano imetekeleza majukumu yafuatayo:

i. Kuanza maandalizi ya kuhuisha Sera ya Mawasiliano ya Simu ya Mwaka 1997 na Mkakati wa Utekelezaji wa Sera ya Taifa ya TEHAMA.

ii. Kuendelea kuratibu ujenzi wa jengo la Makao Makuu ya Umoja wa Posta la Afrika (Pan Africa Postal Union – PAPU) jijini Arusha lenye urefu wa ghorofa 18. Ujenzi wa jengo kwa ujumla wake umefikia asilimia 65;

iii. Kuendeleza mashirikiano ya Kikanda na Kimataifa ambapo Wizara imeshiriki Mkutano Mkuu wa Umoja wa Posta Duniani (UPU) uliofanyika tarehe 9 – 27 Agosti, 2021 Abidjan, Ivory Coast; ambapo chaguzi mbalimbali za viongozi na Mabaraza zilifanyika na Tanzania kufanikiwa kushinda nafasi ya Ujumbe wa Baraza la Utawala ; na Baraza la Uendeshaji la Posta kwa kipindi cha miaka minne (2021 - 2025). Sambamba na hilo, Tanzania imepata nafasi ya Kuongoza Kamati ya Huduma za Posta na Biashara Mtandao ya Umoja wa Posta Duniani.

iv. Kuendelea kuratibu jitihada za ufikishaji wa huduma za mawasiliano ya simu katika maeneo ambayo bado hayajafikiwa na yenye mawasiliano hafifu. Masuala yaliyofanyika ni pamoja na: ukaguzi wa hali ya mawasiliano katika maeneo mbalimbali ikiwemo eneo la Pori Tengefu la Loliondo lenye kata 15, visiwa 171 vya Ziwa Victoria, maeneo ya Kanda ya Ziwa, Kanda ya Juu Kusini, Kanda ya Kati na Pwani. Maeneo yaliyobainishwa yatafikishiwa huduma kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote. Aidha, katika kuratibu jitihada hizi za ufikishaji wa huduma za mawasiliano, Wizara imeandaa Mkakati wa Kuimarisha Mawasiliano wa kipindi cha miaka minne (2021/22 - 2024/25) ili kuboresha huduma za mawasiliano nchini.

v. Kufanya mapitio ya sekta ndogo ya utangazaji na mfumo wa leseni ili kuweka mazingira wezeshi kwa maendeleo ya sekta..

vi. Wizara imetoa leseni 25 kwa ajili ya kutoa huduma mbalimbali kupitia Sekta ya Mawasiliano na TEHAMA.

## Eneo la Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA)

Katika mwaka wa fedha 2021/22 Wizara imetekeleza majukumu yafuatayo:-

i. Kukamilisha uaandaaji wa Mkakati wa Taifa wa intaneti yenye kasi (National broadband Strategy)

ii. Kuandaa mwongozo wa kitaifa wa kushughulikia masuala ya uhalifu wa mtandao unaoongeza uratibu wa pamoja kwa taasisi zote zinazoshughulikia masuala ya uhalifu ya kimtandao.

iii. Kuingia Mkataba wa mashirikiano na TANESCO kwa ajili ya kufanya kazi pamoja ya kupitisha miundombinu ya mawasiliano kwenye nguzo za umeme kwa lengo la kuongeza mtandao wa mawasiliano na wa umeme. Hatua hii imepunguza gharama za ujenzi wa Mkongo na kuharakisha mradi huu ambapo zilikuwa zijengwe Kilomita 1,880 lakini kutokana na Mkataba huu zitajengwa Kilomita 4,442 na kufikisha jumla ya Kilomita 12,761 za Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano

iv. Kuratibu utengenezaji wa mfumo wa kutunza na kuchakata taarifa za kesi na matukio ya uhalifu wa usalama mtandao "cybercrimes module" inayowezesha matukio ya uhalifu kutunzwa na kufuatilia mwenendo wa mashtaka husika hadi kukamilika kwake

v. Kutoa mafunzo kwa waendesha mashtaka, wachunguzi na wapelelezi 197 pamoja na mafunzo ya kutumia "cybercrimes module" kwa watumishi 470 wa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka

vi. Kukamilisha uandaaji wa rasimu ya Mkakati wa Uchumi wa Kidijitali (Digital Economy Strategic Framework) kwa ajili ya kuchochea matumizi ya TEHAMA kwenye sekta zote za uchumi

vii. Kukamilisha uandaaji wa Mwongozo wa Mageuzi ya Kidijitali (Digital Transformation Guideline) kwa ajili ya kutoa mwongozo wa Taasisi zote nchini wa kuelekea uchumi wa kidijitali

viii. Kukamilisha uandaaji wa Programu ya Mafunzo ya TEHAMA yatakayopelekea kuongeza ujuzi na ubobezi wa wataalamu wa ndani ili kuendana na mahitaji ya sasa ya Uchumi wa Kidijitali

ix. Ukamilishwaji wa Mkakati wa Taifa wa Elimu kwa Umma wa Usalama Mtandao (National Cyber Security Communication Strategy), 2021/22 – 2024/25

x. Kukamilisha na kuingia Makubaliano ya Ushirikiano kwenye maeneo ya TEHAMA na nchi ya Rwanda. Aidha, majadiliano na nchi za Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Uganda, Kenya, Marekani, Ujerumani, Uturuki na Falme za Kiarabu yanaendelea

xi. Kuanza mchakato wa kuhamishia shughuli za ujenzi, usimamizi na uendeshaji wa Mkongo wa Taifa wa mawasiliano kwa Shirika la Mawasiliano la Taifa (TTCL).

Katika Mwaka wa Fedha 2022/23 Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari inatarajia kutekeleza majukumu yake kama ifuatavyo:-

i. Kukamilisha uandaaji wa Mkakati wa Kitaifa wa Uchumi wa Kidijitali (National Digital Economy Strategy) na kusimamia utekelezaji wake

ii. Kuratibu na kuwezesha ujenzi wa Mfumo wa TEHAMA kuratibu utendaji kazi wa Wizara

iii. Kusimamia utekelezaji wa Mkakati wa Kitaifa wa Usalama wa Mitandao (National Cyber Security Strategy)

iv. Kusimamia utekelezaji wa Mkakati wa Mtandao wa TEHAMA wenye kasi zaidi (National Broadband Strategy)

v. Kuendelea kuwaendeleza wataalamu 200 kwenye maeneo ya TEHAMA yenye uhaba wa ujuzi

vi. Kuandaa na kusimamia utekelezaji wa Miongozo ya kuimarisha masuala ya utafiti na ubunifu katika TEHAMA

vii. Kuendelea kuimarisha usalama wa mitandao, kuongeza udhibiti wa taarifa binafsi na kupunguza uhalifu wa mitandao kwa kushirikiana na Vyombo vya Usalama

viii. Kuimarisha mashirikiano na mashirika ya mawasiliano ya Kikanda na Kimataifa

ix. Kukamilisha mchakato wa kuhamishia ujenzi,usimamizi na uendeshaji wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano kwa Shirika la Mawasiliano nchini (TTCL)

x. Kupitia upya utaratibu unaotumika katika usimamizi wa Data Center.

## Mradi wa Ujenzi wa Mkongo wa Taifa.

Mradi wa Ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano umekusudiwa kupanua mawasiliano ya simu na intaneti nchini na nchi zinazotuzunguka katika kufanikisha mapinduzi ya kidijitali. Katika kipindi kinachoishia Mwezi Aprili, 2022 kazi zifuatazo zimefanyika:

i. Kukamilika kwa ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano Kilomita 265 (Itigi – Manyoni - Rungwa);

ii. Kukamilika kwa Ujenzi wa Kilomita 72 za Mkongo wa kuunganisha Ofisi za Serikali (Kikombo – Mtumba – Msalato)

iii. Kukamilika kwa Ujenzi wa Kilomita 72 za Mkongo wa Taifa kwenye eneo la Mtambaswala kuunganisha Tanzania na Msumbiji

iv. Kukamilika kwa Upembuzi yakinifu kuunganisha Mkongo wa Taifa na nchi ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) na nyaraka ya zabuni zimeandaliwa;

v. Kukamilika kwa kazi ya kukarabati Kilomita 105 za ujenzi wa mkongo Arusha – Namanga kupitia miundombinu ya TANESCO

vi. Kukamilika kwa Ujenzi wa Kituo cha Kutolea Huduma za Mkongo wa Taifa kwenye Mji wa Serikali Mtumba

vii. Kukamilika kwa taratibu za manunuzi za kuwezesha ujenzi wa Kilomita 4,442 za Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano, upanuzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano kutoka kiwango cha 200G hadi 800G na kujenga vituo vipya 37 na upanuzi wa vituo 75 vya kutolea huduma za Mkongo ambapo mikataba 22 yenye thamani ya Shilingi Bilioni 141 imesainiwa. Aidha, utekelezaji huu utafikisha Mkongo katika Wilaya 23 nchini

viii. Kukamilika kwa Upanuzi wa Mkongo wa Taifa kwenye vituo 5 vya Kigoma, Arusha, Babati, Tunduma na Mbeya vyenye jumla ya kadi za kuchakata huduma (line processing cards) 30;na

ix. Kukamilika kwa kazi ya kuhamisha Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano wenye urefu wa Mita 250 eneo la

Mkazi – Katavi kutokana na kujengwa kwenye eneo la makazi ya watu.

Wizara imeanza mchakato wa kuhamishia shughuli za Kujenga na kuendesha Mkongo wa taifa wa mawasiliano kwa Shirika la mawasiliano nchini TTCL. Mchakato huu utakamilika mwanzoni mwa mwaka wa fedha wa 2022/2023.

Katika Mwaka wa Fedha 2022/23 Wizara imekadiria kutumia Shilingi 149,700,000,000 ambapo Shilingi 149,000,000,000 ni fedha za ndani na Shilingi 700,000,000 ni fedha za nje kwa ajili ya kutekeleza kazi ya ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano. Fedha hizi zitatumika kujenga Kilomita 1,600 za Mkongo na Vituo vipya 15 vya kutolea huduma za Mkongo ili kuongeza wigo wa utoaji wa huduma za Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano hadi kufikisha ngazi za Wilaya nchini. Ujenzi huu utawezesha kufikisha huduma za Mkongo kutoka Wilaya 81 kati ya Wilaya 139.

## Shughuli nyingine zitakazotekelezwa kwenye Mradi huu ni:

i. Kufanya Ujenzi wa Mkongo wa majini kiasi cha Kilomita 60 kuunganisha Tanzania na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo kupitia Ziwa Tanganyika

ii. Kufanya tathmini ya Ujenzi wa Kituo cha kuhifadhi Data Zanzibar

iii. Kuwajengea uwezo wataalam 150 kwenye TEHAMA

iv. Kuendelea kuimarisha usalama wa mitandao, kuongeza udhibiti wa matumizi ya taarifa binafsi na kupunguza uhalifu wa mitandao kwa kushirikiana na Vyombo vya Ulinzi na Usalama;

v. Kukamilisha Nyaraka za Baraza la Mawaziri kuhusu Mapendekezo ya Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi, Sheria ya TEHAMA na Mkataba wa Jumuiya ya Umoja wa Afrika wa Usalama wa Mtandao na Ulinzi wa Taarifa Binafsi (Malabo Convention);

vi. Kuelimisha umma kuhusu Mkakati wa Usalama Mtandaoni

vii. Kuwezesha utendaji kazi wa Kamati za Kiufundi kwa ajilii ya usimamizi wa Mradi wa Mkongo wa Taifa wa mawasiliano;

viii. Kufanya ufuatiliaji na tathmini ya mradi pamoja na ununuzi wa vitendea kazi kwa ajili ya usimamizi wa mradi; na

ix. Kuandaa Mpango Mkuu (Master Plan) wa utekelezaji wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano.

## Mfumo wa Anwani na makazi (Postikodi)

Kufuatia malengo ya Serikali ya kukamilisha Anwani za Makazi kabla ya Sensa ya Watu na Makazi itakayofanyika Mwezi Agosti, 2022, katika Kikao kazi cha Wakuu wa Mikoa kilichofanyika tarehe 08 Februari, 2022; Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan alielekeza Mfumo wa Anwani za Makazi kutekelezwa kwa Mfumo wa Operesheni, aliyoipa jina la “OPERESHENI ANWANI ZA MAKAZI”. Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Ofisi ya Rais – TAMISEMI zimeendelea na utekelezaji wa Mradi chini uratibu wa Ofisi ya Waziri Mkuu.

Katika Mwaka wa Fedha 2021/22 shughuli nyingine zilizotekelezwa ni pamoja na:

i. Kuunda Programu Tumizi (Mobile application) ya Mfumo iliyoongeza ufanisi katika matumizi na utekelezaji wa Mfumo. Programu Tumizi imetumika katika kukusanya taarifa za barabara/ mitaa/ njia, makazi na wakazi sambamba na kumuongoza mtu kutoka anwani ya makazi moja kwenda anwani ya makazi nyingine;

ii. Semina ya kujenga uelewa kuhusu Mfumo wa Anwani za Makazi imetolewa kwa Viongozi 483 ambao ni Wakuu wa Mikoa; Katibu Tawala wa Mikoa; Wenyeviti na Wakurugenzi wa Halmashauri; na Wajumbe wa ALAT; sambamba na Wataalam 616 wa Mikoa na Halmashauri

iii. Hadi kufikia tarehe 18 Mei, 2022 jumla ya anwani za makazi 12,339,471 zimekusanywa na kuingizwa kwenye Programu Tumizi. Idadi ya Anwani zilizokusanywa ni asilimia 106.53 ya lengo la jumla ya Anwani 11,583,564 zilizopangwa kukusanywa katika Mikoa yote nchini. Aidha, kazi ya kuweka miundombinu ya Anwani za makazi inaendelea kote nchini ambapo jumla ya nguzo mpya 74,040 zimesimikwa kati ya 672,952 zinazotarajiwa sawa na asilimia 11 kwa makadirio ya chini kwa wastani wa nguzo 2 kwa kila barabara na jumla ya vibao vya namba za nyumba 906,206 vimebandikwa kati ya 10,537,253 vinavyohitajika sawa na asilimia 9 kama ilivyokuwa jana tarehe 18

Mei, 2022.

Katika Mwaka wa Fedha 2022/23 Wizara imekadiria kutumia Shilingi 40,000,000,000 fedha za ndani kwa ajili ya kuendelea na utekelezaji wa Mfumo wa Anwani za Makazi. Shughuli zitakazotekelezwa ni pamoja na:

i. Kuhakiki miundombinu iliyowekwa wakati wa Operesheni Anwani za Makazi ili kuhakikisha viwango vimezingatiwa

ii. Kuhakiki taarifa zilizokusanywa kwenye Operesheni Anwani za Makazi

iii. Kuboresha Kanzidata na Programu Tumizi ya Mfumo

iv. Kuendelea kuunganisha Mfumo wa Anwani za Makazi na Mifumo mingine ya kutoa huduma za kijamii

v. Kutoa elimu kwa umma; makundi maalum ya kijamii kuhusu manufaa na matumizi sahihi ya Mfumo na kujengea uwezo Taasisi za umma na binafsi kutoa huduma kupitia Mfumo

vi. Kutunga Sheria ndogo za kuwezesha ujenzi na matumizi ya Mfumo, mapitio ya Sheria ya EPOCA na Kanuni zake kuwezesha matumizi ya mfumo

vii. Kununua servers mbili (2) kwa ajili ya kuhifadhi taarifa za mfumo na vifaa vya kuwezesha matumizi ya mfumo

viii. Kuandaa mwongozo ya namna mpya ya kufanya biashara kwa kutumia mfumo

ix. Kutengeneza Mkakati wa usimamizi, uendeshaji na uendelezaji wa mfumo

x. Kuwezesha ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa mfumo

## Mradi wa Tanzania ya Kidijitali

Mradi wa Tanzania ya Kidigitali una thamani ya Dola za Marekani Milioni 150 na ulisainiwa rasmi tarehe 19 Agosti, 2021. Mradi huu unalenga kuboresha na kukuza maunganisho ya ndani na ya kimataifa ili kuweza kufikisha huduma za mawasiliano pamoja na utoaji wa huduma mbalimbali za Serikali kwa Wananchi. Vilevile, mradi huu unalenga kuboresha ubunifu pamoja na kuwajengea uwezo wataalam wa TEHAMA nchini.

## Kazi zilizotekelezwa ni:-

i. Ukamilishaji wa ujenzi wa jengo la Ofisi ya Mradi katika eneo la Area D na kuanza kutumika rasmi tarehe 01 Oktoba, 2021

ii. Kukamilisha usanifu na kuandaa mahitaji ya kuwezesha ununuzi wa bando la intaneti ya Serikali (Government internet bandwidth) kwa ajili ya matumizi ya Taasisi za Umma

iii. Kukamilisha usanifu na kuandaa mahitaji kuwezesha kujenga na kuboresha Mtandao wa TEHAMA unaounganisha Taasisi za Serikali (GovNET)

iv. Kukamilisha ukusanyaji wa mahitaji kuwezesha kujenga na kupandisha hadhi minara 150 ya mawasiliano kutoka teknolojia ya 2G kwenda 3G/4G ili kuwezesha huduma za intaneti yenye kasi kwenye maeneo hayo

v. Kukamilisha manunuzi ya vifaa na programu endeshi za kuboresha vituo mahiri vya kuhifadhia Data (National Internet Data Centre - NIDC na Government Data Centre)

vi. Kufanya tathmini ya maeneo ya kujengewa uwezo kwa watumishi wa TEHAMA Serikalini ambapo jumla ya watumishi 450 watapatiwa mafunzo ya muda mfupi na watumishi 50 watapatiwa mafunzo ya muda mrefu

vii. Kufanya maandalizi ya kuwezesha ujenzi wa Chuo cha TEHAMA ambapo eneo lenye ukubwa wa Hekta 400 limepatikana eneo la Nala, Jijini Dodoma.

Mradi wa Tanzania ya Kidijitali unalenga kuleta mabadiliko ya Kidijitali kwa kuwezesha maunganisho ya Kijiditali ya Kikanda na Kimataifa na hatimaye kukuza Uchumi wa Kidijitali (Digital Economy). Matokeo ya mradi huu ni pamoja na kuongeza na kubuni ajira zitakazotokana na ubunifu wa TEHAMA, ukuzaji wa viwanda vidogo vidogo (SMEs na SMMEs); kukuza ustadi wa wataalamu wa ndani ya Serikali na waliopo nje ya Serikali; na kuongeza uwezo wa utoaji wa Huduma za Serikali kwa kuwezesha uwepo wa intaneti bora ya bei nafuu na ya uhakika kwa ajili ya matumizi ya Serikali ili kumnufaisha mwananchi. Mradi huu utaanza kujenga chuo mahiri cha TEHAMA nchini (Digital Technology Institute). Aidha, mradi huu utapelekea Mawasiliano kwenye maeneo mapya 763 ambapo kiasi cha Shilingi Bilioni 111.59 kitatumika kupitia mradi huu.

Katika Mwaka wa Fedha 2022/23 Wizara inakadiria kutumia kiasi cha Shilingi 39,300,000,000 ikiwa ni fedha za nje kwa ajili ya kutekeleza shughuli zifuatazo:-

i. Kujenga kituo kimoja (1) cha kukuza taaluma na

ubunifu katika TEHAMA na vituo vidogo vitano (5) kwenye kila Kanda

ii. Kuwezesha ununuzi, ugavi na ufungaji wa vifaa katika kituo kimoja (1) kikubwa na vituo vidogo vitano (5) vya kukuza taaluma na ubunifu katika TEHAMA

iii. Kuwezesha ununuzi wa 'bandwidth' kwa ajili ya matumizi ya intaneti ya Serikali

iv. Kusimika mitambo kwa ajili ya kuboresha Kituo cha Taifa cha Kutunzia Data (NIDC)

v. Kukarabati vituo 10 vya Huduma Pamoja

vi. Kujenga mfumo wa kitaifa utakaorahisisha ukusanyaji wa takwimu za TEHAMA

vii. Kujenga, kupanua na kuboresha miundombinu iliyopo ya intaneti yenye kasi (broadband) inayomilikiwa na Serikali (GovNET) na kuunganisha taasisi 100 kwenye Miundombinu hiyo na kufikisha taasisi 390 zilizounganishwa

viii. Kutekeleza programu ya uelimishaji umma kuhusu mradi

ix. Kujenga maabara tatu (3) kwa ajili ya kufufua (refurbishment) vifaa vya TEHAMA katika Mikoa ya Arusha, Dar es Salaam na Mwanza

x. Kujenga minara ya mawasiliano 150 kwenye Kata 150 ili kuwezesha huduma za mawasiliano nchini

xi. Kufanya mapitio na kuhuisha Sera, Sheria na Kanuni za Sekta ya TEHAMA

xii. Kuwajengea uwezo wataalam wa TEHAMA nchini kwa kuwapatia watalaam 200 mafunzo ya muda mfupi na wataalam 10 mafunzo ya muda mrefu

xiii. Kufanya tathmini ya kuainisha mahitaji na usanifu wa kujenga mfumo wa kuwezesha biashara mtandao.

## Mradi wa Kuendeleza Ubunifu na Utengenezaji wa Vifaa vya TEHAMA

Katika Mwaka wa Fedha 2022/23 Wizara inakadiria kutumia Shilingi 3,300,000,000 fedha za ndani kwa ajili ya kutekeleza Mradi wa Kuendeleza Ubunifu na Utengenezaji wa Vifaa vya TEHAMA. Fedha hizo zinaombwa kwa ajili ya kutekeleza shughuli zifuatazo:


i. Kujenga Kituo cha Kuendeleza Wataalam, tafiti na ubunifu wa TEHAMA na kufanya maandalizi ya ujenzi wa makao makuu ya Tume ya TEHAMA;

ii. Kukiendeleza kituo cha kuendeleza kampuni changa za TEHAMA (ICT startups) cha Dar es Salaam na kujenga vituo viwili (2) vya Kanda vya kutengeneza bidhaa za TEHAMA;

iii. Kuanzisha Vituo vya Ubunifu na Atamizi TEHAMA katika Wilaya mbili (2) nchini;

iv. Kutengeneza mfumo jumuishi utakaounganisha usajili na uendelezaji wa wataalam na wabunifu TEHAMA nchini (ICT human capital development system); na

v. Kuwezesha shughuli za ufuatiliaji na tathmini ya Mradi.




*Ramani ya Mkongo wa taifa wa mawasiliano. Shilingi 149,700,000,000 zitatumika kutekeleza kazi ya ujenzi wa Mkongo Kilomita 1,600 na Vituo vipya 15 vya kutolea huduma za Mkongo ili kuongeza wigo wa utoaji wa huduma za Mkongo hadi kufikisha ngazi za Wilaya nchini. Ujenzi huu utawezesha kufikisha huduma za Mkongo kutoka Wilaya 81 kati ya Wilaya 139.*

# Vikoa vya dot tz (.tz)

### Kikoa ni nini?

Ni jina mahsusi linalotambua raslimali za intaneti kama vile tovuti zilizosajiliwa nchini na ngazi nyingine duniani.

Kompyuta zilizounganishwa kwenye intaneti zina anwani za namba mahsusi zinazoziwezesha kufikisha taarifa za kielektroniki mahali sahihi. Mfumo wa Majina ya domeini (DNS) unatafsiri anwani hizo za namba kwenye kompyuta na kuzipa majina ambayo ni rahisi kutumiwa. Vikoa vinavyojitokeza ni rahisi kukumbuka na vinasaidia watu kupata taarifa kwenye intaneti.

Vikoa vinatumika kutambua kurasa mahsusi za tovuti. Kwa mfano, katika anwani ya tovuti ya "https://www.tcra.go.tz," kikoa ni tcra.go.tz.

Vikoa pia vinatumiwa katika anwani za barua pepe ambazo zinawezesha watu kutuma na kupokea ujumbe wa kielektroniki; kwa mfano, barua@tcra.go.tz.

Mfumo wa vikoa ni nini?

Kwa lugha nyepesi, mfumo wa vikoa, au DNS in kitabu cha namba za mawasiliano kwa intaneti, unaounganisha watumiaji wa mtandao wa intaneti na tovuti mballimbali.

Mfumo wa vikoa, yaani DNS ni kanzidata iliyojengeka na duniani na ambayo inawezesha mawasiliano kupitia intaneti kwa kutafsiri majina haya ambayo ni rahisi kutumia (vikoa) kuwa misimbo mifupi ya namba (anwani za intaneti) ambazo kompyuta au vifaa vinavyotumika kwenye mtandao vitazielewa; na kinyume chake.

Domeini ya Kiwango cha Juu ya Fumbo la Nchi (ccTLD) ni nini?

Domeini ya Kiwango cha Juu ya Fumbo la Nchi, (kwa ufupi ccTLD) ni domeini ya kiwango cha juu ya fumbo ambacho kawaida kinatumika au kimetengwa kwa nchi, dola huru au eneo la nchi linalotambulika kwa msimbo wa nchi.

Domeini ya kiwango cha juu ya fumbo ina urefu wa herufi mbili; kwa mfano TZ ni Tanzania, KE ni Kenya, UK ni Uingereza.

### Rajisi ni nini?

Rajisi inafanya kazi kama hazina ya yenye mamlaka inayohifadhi taarifa zote zinazotakiwa kutoa ufumbuzi wa vikoa vilivyosajiliwa kwenye domeini ya kiwango cha juu ya fumbo (TLD) na rajisi hiyo au domeini za ngazi ya pili (SLDs) iwapo mfumo wa SLD unatumika (kwa mfano co.tz, ac.tz).

Rajisi hiyo pia inaweka taarifa za ziada kama vile uendeshaji wake na utaratibu wa kiufundi wa kuwasiliana nayo, namna ya kuwasiliana na domeini husika, utaratibu wa mawasiliano kwa ajili ya ankara na mrajisi aliyesajili kikoa hicho.

### Msajili ni nani?

Ni mtu au taasisi iliyopewa kibali na Mamlaka kusajili, kufuta, kuongeza, kurekebisha au kubadili vikoa chini ya utaratibu wa vikoa vya dot tz (.tz).

### Msajiliwa ni nani?

Huyu ni taasisi au mtumiaji binafsi ambaye anasajili kikoa.

Meneja wa domeini ya kiwango cha juu ya fumbo (ccTLD) ni nani?

Meneja (ccTLD) ni taasisi (kampuni) au mtu binafsi ambaye anashughulikia masuala ya kila siku ya Domeini ya Kiwango cha juu ya Fumbo au shughuli zinazoambatana nayo kwa niaba ya jumuiya ya intaneti alipo.

Mamlaka inayokasimu majukumu kwa Meneja wa Domeini ya Kiwango cha juu ya Fumbo ni taasisi ya kimataifa inayosimamia masuala ya intaneti, inayoitwa ICANN, ambacho ni kifupisho cha Internet Corporation for Assigned Names and Numbers.

Kwa kikoa cha dot tz (.tz) cha ccTLD, meneja ni Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania.

### Domeini ya ya Fumbo ngazi ya Pili ina aina zipi?

Majina ya Domeini ya ya Fumbo ngazi ya Pili ni kama ifuatavyo:

- <jina>.co.tz – kwa taasisi yoyote, ikiwa ni pamoja na kampuni au biashara zilizosajiliwa;
- <jina>.or.tz – taasisi zisizojiendesha kibiashara;
- <jina>.go.tz – domeini iliyotengwa kwa taasisi za Serikali ya Tanzania kama zinavyotambuliwa kupitia Bunge au kwa kuwa na barua kutoka kwa Katibu Mkuu wa Wizara husika ilipo taasisi hiyo;
- <jina>.ac.tz– domeini iliyotengwa kwa vyuo vya elimu au taasisi za ufundi zenye usajili kama ipasavyo;
- <jina>.ne.tz – kwa mtandao wa watu au bidhaa;
- <jina>. mil.tz – domeini iliyotengwa kwa taasisi za kijeshi za Tanzania zinazotambuliwa na Wizara yenye majukumu ya Ulinzi.
- <jina>.sc.tz – domeini iliyotengwa kwa shule za awali, msingi na taasisi za ngazi ya sekondari;
- <jina>. info.tz – kwa domeini zinazotoa habari kuhusu masuala mahsusi;;
- <jina>.tv.tz – kwa matumizi ya watunza maudhui, watengenezaji wa filamu na stesheni za televisheni;
- <jina>. mobi.tz – kwa watoa huduma kupitia vifaa vya mkononi;
- <jina>. hotel.tz – kwa watoa huduma za malazi na ukarimu; na
- <jina>.me.tz – kwa watu binafsi.